HOTUBA YA MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (MB), NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA, ALIYOITOA KWENYE MKUTANO NA WATENDAJI WA TAASISI ZA UMMA KATIKA MKOA WA MWANZA TAREHE 02 OKTOBA, 2019

Mheshimiwa John V. K. Mongella, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza,
Wastahiki Meya Halmashauri ya Jiji na Manispaa za Mwanza,
Mheshimiwa Balozi (Mstaafu) John M. Haule,
Mheshimiwa Khadija A.M. Mbarak,
Mheshimiwa Alhaj Yahya F. Mbila, Makamishna wa Tume,
Ndugu Nyakimura M. Muhoji, Katibu wa Tume,
Ndugu Christopher D. Kadio, KatibuTawala wa Mkoa wa Mwanza,
Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Mwanza,
Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma katika Mkoa wa Mwanza,
Makatibu Tawala wa Wilaya za Mkoa wa Mwanza,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana,
Habari za asubuhi,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha baadhi yetu kusafiri salama na kufika hapa ili kushiriki Kikao hiki cha kazi ambacho ni muhimu sana. Lengo kuu la Kikao hiki ni kujifunza na kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi katika uendeshaji na usimamizi wa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma. Aidha, napenda

kuushukuru uongozi wa Tume ya Utumishi wa Umma na wote walioshiriki katika kuandaa kikao hiki na kuhakikisha kuwa ziara hii inafanyika kama ilivyopangwa.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Maelezo ya utangulizi ya Kamishna yameainisha majukumu na changamoto mbalimbali ambazo Tume ya Utumishi wa Umma inakutana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yake, yakiwemo ya kupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na ya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu na Miongozo mbalimbali katika usimamizi na uendeshaji wa Rasilimali Watu. Kutokana na maelezo hayo tumepata picha kwamba bado Waajiri wengi, Mamlaka za Ajira na Nidhamu hazizingatii Sheria, Kanuni na Taratibu katika kushughulikia masuala yanayohusu ajira na mashauri ya nidhamu ya watumishi walio chini yao.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Tumeelezwa hapa kuwa baadhi yenu hamzingatii taratibu za ajira mpya; watumishi wapya hawapewi mafunzo elekezi; kutowathibitisha kazini kwa wakati watumishi baada ya kumaliza kipindi chao cha majaribio na watumishi kutopewa mgawanyo wa majukumu wanayotakiwa kutekeleza. Hii inasababisha watumishi kutozifahamu Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo na majukumu yao na hatimae kukiuka Miiko na Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Kuchelewa kuwathibitisha kazini kunawanyima watumishi haki na stahili zao mbalimbali hivyo, kusababisha malalamiko yasiyo ya lazima na kupunguza ari ya utendaji kazi.

Aidha, nawaagiza Waajiri wote kuhakikisha kuwa waajiriwa wapya wanapewa mafunzo elekezi, kuwawezesha kufahamu majukumu ya kazi wanazotakiwa kutekeleza na miiko na maadili ya Utumishi wa Umma.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Changamoto nyingine iko kwenye upandishwaji vyeo. Baadhi ya Waajiri na Mamlaka za Ajira zinawapandisha vyeo Watumishi bila kuzingatia Tange (Seniority List) na bila kuwepo kwa taarifa za utendaji kazi (OPRAS) za miaka mitatu mfululizo kama maelekezo ya Waraka wa Katibu Mkuu UTUMISHI wenye Kumb. Na. CBD.45/352/01/26 wa tarehe 01/08/2012.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Suala la ujazaji wa OPRAS ni takwa la kisheria kama inavyobainishwa na Kifungu cha **6** cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya **298.** Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, suala hili bado halipewi umuhimu unaostahili. Taarifa za Kaguzi mbalimbali zinazofanywa na Tume kuhusu usimamizi na uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu zinaonesha kuwa suala la OPRAS bado lina changamoto kubwa kiutekelezaji. Maeneo ambayo bado yameonekana kutofanya vizuri ni pamoja na watumishi kutojaza kabisa OPRAS; kutozingatiwa kwa vipindi vya ujazaji wa OPRAS; watumishi kutopewa mgawanyo wa kazi; malengo ya utendaji kazi kutokuwa "SMART"; alama za utendaji kazi kutokokotolewa kikamilifu; na kutokujaza fomu za OPRAS kwa ukamilifu.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Kupitia kikao hiki, ninatoa, maagizo yafuatayo: Kwanza, kila Mwajiri ahakikishe kuwa watumishi wake wanapata elimu kuhusu dhana nzima ya OPRAS ili waweze kuielewa na kuitekeleza kikamilifu; Pili, kila Mwajiri ahakikishe kuwa watumishi wake wanajaza OPRAS kikamilifu na kufanya tathmini ya utendaji kazi wao ili kuhakikisha kwamba malengo iliyojiwekea Taasisi yanafikiwa; Waajiri nao wahakikishe kwamba wanawapa watumishi wapya walioajiriwa na waliopandishwa vyeo mgawanyo wa kazi ili waweze kujaza malengo ya utendaji kazi kulingana na majukumu yao.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Kuhusu masuala ya nidhamu tumeelezwa kwamba baadhi ya Mamlaka za Nidhamu haziyashughulikii kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Upungufu uliobainishwa ni pamoja na kutokuwepo kwa Rejista za mashauri ya nidhamu; watumishi watuhumiwa kutopewa fursa ya kuwahoji mashahidi; barua za uamuzi kujumuisha makosa ambayo hayamo kwenye Hati ya Mashtaka; kutoteua Kamati za Uchunguzi au Kamati kuundwa na Wajumbe wasiokuwa na sifa stahiki au Kamati za Uchunguzi kutokuteuliwa na Mamlaka halali; na uamuzi wa shauri kuchelewa kutolewa na wakati mwingine kutolewa na Mamlaka isiyo halali kisheria, mfano Mkurugenzi wa Halmashauri kumfukuza mtumishi badala ya Baraza la Madiwani, au Katibu Tawala Msaidizi badala ya Katibu Tawala wa Mkoa.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Kitendo cha Mamlaka za Nidhamu kutokuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wa kushughulikia masuala ya nidhamu kinaisababishia Serikali hasara pale inapolazimika kuwalipa watumishi mishahara ambayo hawakuifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuanzishwa upya kwa mashauri ya nidhamu na watumishi kurejeshwa kazini. Hivyo, nawaagiza Watendaji Wakuu wa Taasisi zote za Umma kuhakikisha kwamba mashauri ya nidhamu yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Wale ambao watakiuka Tume ya Utumishi wa Umma izijulishe Mamlaka zao za Nidhamu ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao mara moja.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Ili haki itendeke na ionekane kweli inatendeka ni lazima itolewe kwa wakati. Tume ya Utumishi wa Umma imepewa mamlaka kisheria ya kuwataka Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuwasilisha vielelezo mbalimbali kuhusu rufaa na malalamiko ya Watumishi pale vinapohitajika. Baadhi yenu mnachelewa kuwasilisha vielelezo husika bila sababu za msingi. Hali hii husababisha Tume kuchelewa kushughulikia rufaa na malalamiko ya watumishi na kuleta usumbufu na gharama kwa watumishi husika na Tume kwa ujumla. Ninaagiza, Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu na wadau wengine wote, mhakikishe mnawasilisha vielelezo Tume kwa wakati pale mnapotakiwa kufanya hivyo ili haki itolewe kwa wakati.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Watumishi wa Umma wanapowasilisha rufaa na malalamiko mbele ya Tume, jukumu la Tume ni kutoa uamuzi kuhusiana na rufaa na malalamiko husika. Jukumu la Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu ni kutekeleza uamuzi wa Tume na pale ambapo hazijaridhika, zinapaswa kukata rufaa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya siku arobaini na tano tangu tarehe ya kupokea uamuzi husika. Hata hivyo, baadhi ya Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu huchelewa au hazitekelezi kabisa maagizo ya Tume. Kutotekeleza maagizo ya Tume ni ukiukwaji mkubwa wa sheria na kitendo hiki husababisha usumbufu mkubwa kwa Tume kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake na kwa Warufani ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu kujua hatma ya rufaa zao. Hivyo, kupitia Kikao hiki, ninawataka Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuzingatia maelekezo ya sheria kwa ama kutekeleza maagizo ya Tume au kukata rufaa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 10 (2), cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura **298**, Tume imepewa mamlaka ya kisheria ya kuwataka Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma kuwasilisha Tume taarifa kuhusu masuala mbalimbali ya uendeshaji wa Rasilimali Watu. Taarifa hizi ni chanzo kimojawapo kinachoonesha hali ya Utumishi wa Umma Nchini ili kuisaidia Serikali katika mipango yake kwenye masuala ya kiutumishi. Tumeambiwa kuwa katika kipindi cha mwaka **2017/2018** hali ya uwasilishaji wa taarifa Tume kutoka Taasisi zilizoko katika Mkoa wa Mwanza ilikuwa si ya kuridhisha. Ninatoa

maelekezo kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuhakikisha kuwa zinawasilisha Tume Taarifa za Kiutumishi za kila robo mwaka kwa wakati. Kwa hili naiagiza Tume kutekeleza wajibu wake na itumie vilivyo Mamlaka iliyopewa, ihakikishe Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu wanawasilisha taarifa zao kwa wakati na kunipatia taarifa kwa Taasisi zitakazoshindwa kutekeleza agizo hili.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Taarifa za Ukaguzi wa Uendeshaji na Usimamizi wa Rasilimali Watu kwa mwaka **2017/2018** na **2018/2019** zinaonesha kuwa eneo lingine ambalo halisimamiwi ipasavyo ni eneo la mafunzo kwa Watumishi wa Umma. Baadhi ya upungufu uliobainishwa ni pamoja na kutofanyika kwa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo; Taasisi kutokuwa na Mpango wa Mafunzo; watumishi waliopo masomoni kutokuwa na ruhusa za kwenda masomoni; na Watumishi kwenda mafunzo bila kuwepo kwenye Mpango wa Mafunzo.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Lengo la mafunzo ni kuwaongezea watumishi ujuzi na stadi za kazi kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija. Lakini kutokuwa na Mpango wa Mafunzo kuna athari kwa Taasisi, kama vile watumishi wengi kuomba na kuruhusiwa kwenda masomoni wakati wowote hivyo, kuathiri utendaji kazi wa Taasisi; watumishi kusoma kozi ambazo hazina tija kwa Taasisi zao; na malalamiko ya upendeleo pale ambapo mtumishi mmoja ataruhusiwa kwenda masomoni na mwingine akakataliwa kwa sababu hakukuwa na vigezo vya uchaguzi huo. Kupitia Kikao hiki, ninatoa maagizo kuwa, kila Taasisi ihakikishe inafanya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo (Training Needs

Assessment), inaandaa Mpango wa Mafunzo na inafanya Tathmini ya Utekekelezaji wa Mpango wa mafunzo kila mwaka.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Ninafahamu kuwa baadhi ya Wakuu wa Taasisi za Umma hawajibu kwa wakati au hawajibu kabisa barua za Watumishi wao kuhusiana na maombi au madai mbalimbali. Suala hili pia husababisha watumishi kulazimika kuzunguka huku na kule kujaribu kupata ufumbuzi wa kero zao badala ya kufanya kazi. Hali hii pia huleta usumbufu kwa Viongozi wa Ofisi zingine ambao watumishi husika hulazimika kupeleka malalamiko yao kwao. Ieleweke wazi kwamba, kujibu barua za watumishi sio hiari bali ni takwa la kisheria. Ninasisitiza, Waajiri wote kuzingatia maelekezo ya sheria ili kuondoa kabisa kero hii.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Katika siku za hivi karibuni tumekuwa tukishuhudia siri za Serikali zikivuja kinyume na Kifungu cha **4** Sheria ya Usalama wa Taifa Na. **3** ya mwaka **1970.** Nitumie fursa hii kusisitiza kuhakikisha kuwa watumishi wenu wanajaza Fomu za Maadili ya Utumishi wa Umma na kuchukua hatua mara moja pale ukiukwaji unapotokea.

Ndugu Viongozi wa Taasisi za Umma,

Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kuwa, tunazo rasilimali mbalimbali zikiwemo Rasilimali Watu, Rasilimali Fedha, Rasilimali Muda na Rasilimali Vitu. Hata hivyo, rasilimali iliyo na umuhimu wa kwanza kati ya hizo ni Rasilimali Watu kwa kuwa ndiyo inayozisimamia na kuziendesha rasilimali zote

hizo. Hivyo, kila mmoja katika eneo lake akisimamia watumishi walio chini yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuifikisha Tanzania kwenye Uchumi wa Kati, itafanikiwa.

INAWEZEKANA KUWA NA UTUMISHI ULIOTUKUKA, TUWAJIBIKE.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.